***Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne. Chagua jibu lifaalo zaidi kati ya yale uliyopewa.***

____1_____ ya Zainabu yalipomfika ____2___, hakuwa na budi kuwasaka ____3____ ili kuinusuru hali. Awali, alijaribu kwa ____4____ kuyaficha huku akisahau kuwa ____5____. ____6____ angaliyazingatia ya washauri ya kuvalia barakoa _____7____ katika maeneo ya umma na kuepuka halaiki. Hata hivyo, ya kumwagika yameshamwagika . Yamkini, _____8____ itamsafirisha jongomeo.

**1.** A. Magonjwa B. Ugonjwa C. Maradhi D. Uele
**2.** A. koo B. kooni C. mwilini D. mwili
**3.** A. maafisa wa afya B. watetezi wa haki C. waganga na waganguzi D. makungwi na manyakanga
**4.** A. inda na tadi B. udi na uvumba D. wasiwasi na woga D. heri na shari
**5.** A. afichaye ugonjwa haponi
B. gangaganga za mganga humlaza mgonjwa na matumaini
C. mficha uchi hazai
D. sitafuga ndwele na waganga wa tele
**6.** A. Aghalabu B. Kama C. Endapo D. Laiti
**7.** A. awapo B. wakiwa C. akikuwa D. anapokua
**8.** A. malaria B. homa C. ugonjwa D. Korona

Kadiri uchaguzi mkuu unavyokaribia, ndivyo vigogo wengi _____9_____ kujitosa ulingoni huku kila mmoja akiwania kuushika usukani ____10_____. Wengi wameonekana katika vyombo vya habari ____11____ na kuahidi uongozi _____12____ pindi wapewapo fursa. Tatizo ni kuwa, badala ya ____13___, ____14____ kati ya mirengo hii ya kisiasa imeshuhudiwa ikisambaratika viongozi wakuu humo wakibaidika kama ____15____. Yote tisa, kumi, naije heri. Kusiwe na umwagikaji wa . damu.

**9.** A. wanavyozidi B. wanazidi C. wanapomaliza D. wakianza
**10.** A. mwaka huu B. mwezini C. mwezi huu D. mwakani
**11.** A. wakijiuma vyanda B. wakijitia hamnazo C. wakijipiga vidari D. wakijipurukusha hadharani
**12.** A. nzuri B. bora C. njema D. duni
**13.** A. kutengana B. utengano C. utangamano D. kutenga
**14.** A. mingi B. wengi C. nyingi D. vingi
**15.** A. ambari za zinduna B. moto wa kifuu C. kiko na digali D. ardhi na mbingu

***Kutoka swali la 16 hadi 30, jibu kulingana na maagizo.***

16. Tambua sentensi iliyotumia O-rejeshi ya tamati kwa usahihi.
A. Porini kuna wanyama walao watu.
B. Porini kuna wanyama wakulao watu.
C. Porini kuna wanyama wanaokula watu.
D. Porini kuna wanyama wanaowala watu.

17. Kanusha sentensi ifuatayo kwa ustadi:
**Ungeliona gazeti ungelisoma.**
A. Hungeliona gazeti hungelisoma.
B. Usingaliona gazeti usingalisoma.
C. Usingeliona gazeti usingelisoma.
D. Ungeliona gazeti usingelisoma.

**18.** Maneno kama vile **bawaba na bawabu na mchuzi na mchuuzi** huitwa
A. viambishi B. vitate
C. visawe D. vitawe

**19.** Chagua kiunganishi bora zaidi kukamilishia sentensi:
**Simwogopi nyoka**
A. ingawa mjusi. B. angaa mjusi.
C. aghalabu mjusi. D. sembuse mjusi.

**20.** Mtu afanyaye makosa kama ya wengine ila huishia kuyaona hayo ya wengine bila kuona yake husutwa kwa methali gani?
A. Kosa moja halimwachishi mke.
B. Nyani haoni kundule.
C. Angalipaa juu kipungu hafikilii mbinguni.
D. Doa usoni huonekana kwa kioo.

**21.** Chagua ukubwa wa sentensi hii.
**Watoto wa ng'ombe wanaitwa ndama.**
A. Matoto ya magombe yanaitwa madama.
B. Watoto wa ng'ombe wanaitwa ndama.
C. Toto la gombe linaitwa dama.
D. Vitoto vya vigombe vinaitwa vidama.

**22.** **Kukata kiu** ni sawa na
A. kuaga dunia B. kunywa maji
C. kula chakula D. kuenda mbio

**23.** Kutokana na kitenzi **changamka**, tunaweza kuunda sifa gani?
A. Changamkia B. Kuchangamka
C. Uchangamfu D. Changamfu

**24.** Je ni kauli ipi inayoonyesha mnyambuliko wa kitenzi katika hali ya kutendesha?
A. Mtoto alimlilia mama yake.
B. Tulipeleka magodoro bwenini.
C. Yaya amemlaza mtoto.
D. Babu amelifungua dirisha.

**25.** Ni kipi kinyume cha:
**Msichana ataenda jioni?**
A. Kijana atakuja asubuhi.
B. Mvulana atakuja asubuhi.
C. Msichana hataenda jioni.
D. Mvulana hatakuja jioni.

**26.** Chagua kiambishingeli bora zaidi kujazia pengo.
**Siku ___ona ufagio uani.**
A. u B. i
C. li D. zi

**27.** Chagua sentensi sahihi kisarufi.
A. Watoto ambao wachezao ndio wetu.
B. Mimi ndiyo nilinunua mpira.
C. Ambaye ana bidii ndiye hufaulu.
D. Dawati ambayo ameikalia si yake.

**28.** Chagua neno lenye maana sawa na lile lililopigiwa kistari.
Waridi ameiwasha **runinga** yake.
A. Jokofu
B. Televisheni
C. Feni
D. Kompyuta

**29.** Nomino **wavu** ipo katika ngeli gani?
A. U - YA B. U - I
C. U - U D. U - ZI

**30.** Ripoti:
**"Nitakuona kesho," mgonjwa alimwambia daktari.**
A. Daktari alimwambia mgonjwa kuwa angemwona siku ambayo ingefuata.
B. Mgonjwa alimwambia daktari kuwa angemwona siku ambayo ingefuata.
C. Daktari aliambiwa na mgonjwa kuwa angemwona kesho.
D. Mgonjwa alisema kuwa atamwona daktari siku iliyofuata.

***Soma kifungu kisha ujibu maswali 31 hadi 40.***

Wenye ndimi za uhenga waliwahi kusema kuwa mkataa pema pabaya panamwita. Kombo alikuwa mvulana mchangamfu na kipenzi cha walimu na wazazi. Kwa bahati mbaya, mambo ya Kombo yalienda kombo. Sasa ni mwehu. Utukutu na ukaidi wake ndilo lililokuwa gari na nauli ya kumsafirisha milima na mabonde, misitu na nyika hadi huko aliko sasa.

Awali wazazi wake walimpa maonyo na nasaha chungu nzima. Hayo yote yaliambulia patupu. Walimu nao wakashindwa la kusema. Katika darasa la sita, Kombo alijiunga na kundi la wanafunzi waliokuwa wameyaasi masomo na kuwa mbwakoko kijijini. Chanzo cha matumizi ya dawa za kulevya kilikuwa uvutaji wa sigara ili kuwafurahisha wenzake ambao tayari walikuwa watumwa wa sigara na bangi.

**<u>Maskini Kombo akawa bendera</u>**. Ili kudumisha urafiki wao, Kombo alianza kutumia dawa nyingine za kulevya. Walimu walipogundua haya, waliwafahamisha wazazi wake mara moja, nao kwa ushirikiano wa kiko na digali, hawakuchelea wala kuchelewa kumpa nasaha na ushauri. Ushauri huo Kombo aliutema kama masuo huku akitia nta masikioni. Mwishowe aliamua kuacha masomo na kujiunga na wenzake. Hatimaye, yeye na wenzake hao wakahamia mjini.

Jijini walijiunga na vibaka na shughuli ikawa ni kuwavizia wapitanjia ili kuchopoa vibeti. Vilio vya kuibiwa vilitanda humo mjini. Waama, aliyekutana na pwagu Kombo baada ya saa moja jioni alijuta kuchelewa alikokuwa. Wizi na matumizi ya mihadarati uliendа sambamba katika maisha ya Kombo. Bangi alizovuta kwa wingi zilisababisha aanze kurukwa na akili polepole. Hatimaye, Kombo alirukwa na akili kabisa na kuwa mwehu au wazimu.

Ndovu hakulemewa na mkonga wake! Wazazi wake walipopata habari na pia kupashwa alikokuwa mwanao, walimwendea. Madaktari walijitahidi kuokoa hali lakini ganga ganga zao hazikumwacha mgonjwa na tumanini lolote.

---

**31.** Kulingana na aya ya kwanza, ni nini kilichochangia hali ya sasa ya Kombo?
A. Gari B. Nauli
C. Kukataa maonyo D. Walimu

**32.** Sifa mbaya ambazo mwandishi anampa Kombo katika aya ya kwanza zilitokana na
A. kukataa pema.
B. kukataa pabaya.
C. kupendwa na walimu na wazazi.
D. kuutilia maanani ushauri.

**33.** Kulingana na aya ya pili, tutakosea iwapo tutasema
A. marafiki zake Kombo walikuwa wametoroka shuleni
B. ushauri wa wazazi ulimfaa sana Kombo
C. walimu walishangazwa na tabia za Kombo.
D. marafiki zake Kombo walikuwa watumizi wa mihadarati.

**34.** Kombo alivuta sigara mwanzoni ili
A. apate nguvu za kufanya kazi shuleni.
B. aweze kuwadharau wavyele na walimu.
C. ajihisi mkubwa kiumri.
D. kuwafurahisha marafiki zake.

**35.** '**<u>Maskini Kombo akawa bendera</u>**' inaleta dhana kuwa Kombo
A. alikuwa na uamuzi imara.
B. aliwafuata wenzake bila hiari.
C. alikuwa na tabia tofauti tofauti.
D. akawa mwepesi wa kufikiri.

**36.** Kombo alianza kutumia dawa za kulevya
A. alipotoroka shuleni.
B. alipoonywa na wazazi wake.
C. alipokuwa angali shuleni.
D. alipofika mjini.

**37.** Nasaha na ushauri ambao Kombo alipewa
A. aliutii barabara.
B. aliukumbatia na kuulinda.
C. aliupenda zaidi.
D. aliupuuza kabisa.

**38.** Kule mjini, Kombo
A. alikuwa mwizi mkubwa.
B. aliimarika kitabia.
C. alipata kazi nzuri.
D. alikuwa na ujuzi mwingi.

**39.** Dhara lililojitokeza wazi katika maisha ya Kombo lilikuwa gani?
A. Kuokolewa na wazazi wake.
B. Kuwa kichaa maisha yake yote.
C. Wazazi na madaktari kushindwa kumsaidia.
D. Yeye kutoroka mjini na wenzake.

**40.** Je, umekutana na methali ngapi katika kifungu hiki?
A. Tano B. Moja
C. Mbili D. Tatu

***Soma kifungu kisha ujibu maswali 41 hadi 50.***

Nchi yoyote ulimwenguni huhitaji kuimarika kiuchumi. Taifa letu lina viwanda tofauti tofauti. Hapa mafundi wenye ujuzi uliokomaa huonyesha ueledi wao wa kuzalisha mali. Bidhaa kutoka viwandani humu huuzwa nchini huku za ziada zikiuzwa nje ya nchi.

Vipo viwanda vya kushona nguo. Cherehani hutumika kushonea nguo kama suti, makabuti, masurupwenye miongoni mwa mavazi mengine mengi. Mara nyingi vyerehani hutumia nguvu ya umeme. Washonaji ambao hawajafanikiwa kupata umeme hutumia mitambo ya jenereta ambayo huzalisha kawi ya umeme.

Leo, viwanda vya sandarusi ni mashuhuri kote nchini. Kutokana na kuadimika kwa mbao, viwanda hivi hutumia plastiki kuzalisha bidhaa kama meza na viti. Bidhaa nyingine kutoka humu ni matangi ya maji ambayo hupatikana katika pembe zote za nchi yetu. Matangi haya yamesaidia sana katika uhifadhi wa maji.

Viwanda vya bidhaa za vyuma navyo ni vingi sana. Pale, utawapata wahunzi mahiri wakizalisha mali. Wao husana bidhaa kama vile sururu, majembe na masanduku. Aidha, vyuma vya ujenzi wa majumba marefu hutoka hapa. Kwa sababu ya ukali wa joto la pale, wao huvalia mavazi mepesi huku wakihakikisha kuwa wamevalia viatu madhubuti vya kulinda nyayo zao. Si ajabu kuwaona wakitiririkwa na jasho kila wakati. Wao hutumia vifaa kama vile nyundo, fuawe, jiriwa na kadhalika.

Vilevile, kunavyo viwanda vya kutenegeneza saruji. Hivi navyo husaidia pakubwa katika ujenzi wa taifa letu. Majumba marefu marefu na imara yamesambaa kote nchini. Saruji ndiyo inayotumiwa na waashi katika ujenzi wa majumba haya. Saruji ya ziada huuziwa mataifa mengine ili kuiletea nchi yetu donge nono.

**41.** Kwa mujibu wa aya ya kwanza,
A. nchi yetu haina viwanda vingi.
B. mafundi humu nchini ni hodari.
C. bidhaa kutoka viwandani hutumika humu nchini tu.
D. weledi ndio wenye viwanda.

**42.** Kulingana na kifungu, lipi **si** zao la viwanda vya kushonea nguo?
A. Surupwenye
B. Kabuti
C. Sare
D. Suti

**43.** Mitambo ya jenereta hutumiwa na
A. wasiopenda umeme.
B. mafundi wasio na ujuzi wa kutosha.
C. wanaozalisha stima
D. wale ambao hawajaunganishwa na umeme.

**44.** Kulingana na mwandishi, sababu ya viwanda kutengeneza meza na viti vya plastiki imechangiwa na
A. uhaba wa mbao
B. wingi wa mbao.
C. ukosefu wa miti
D. mbao kuwa ghali

**45.** Bidhaa ambayo ni nadra kuikosa katika sehemu za nchi ni
A. maji B. matangi
C. viwanda D. majumba

**46.** Ni gani hapa **si** zao la mhunzi kulingana na habari?
A. Sururu
B. Meza
C. Majembe
D. Masanduku

**47.** Tumeambiwa kuwa ule uthabiti wa ghorofa hutokana na
A. vyuma
B. sarufi
C. wahunzi
D. mafundi

**48.** Wahunzi huweza kutumia ala hizi zote **ila**
A. jiriwa
B. nyundo
C. fuawe
D. vyerehani

**49.** Baadhi ya saruji ambayo huzalishwa nchini
A. huiletea nchi yetu pato kubwa sana.
B. ni kichochezi cha uchumi .
C. huuziwa nchi jirani.
D. huhifadhiwa katika maghala makubwa.

**50.** Kichwa **bora zaidi** kwa taarifa hii ni
A. Mafundi hodari
B. Viwanda vya humu nchini
C. Viwanda vya saruji
D. Bidhaa za plastiki